



MASWALI YANAYOULIZWA KILA WAKATI KUTOKA KWA WAZAZI WA KIISLAMU KATIKA DPS

DPS imejitolea kutoa mazingira ya kusoma mbali na ubaguzi na unyanyasaji kinyume na sheria.

Je, mtoto wangu atafahamishwa wakati chakula kina bidhaa ya nguruwe?

Huduma za Chakula na Lishe ilianzisha hivi majuzi ishara ya “nguruwe” ambayo inaonyesha wakati chakula kina bidhaa ya nguruwe. Kwa ujumla, viamsha kinywa na vyakula vya mchana vya DPS huwa havina nguruwe. Unaweza kujadiliana maswali au wasiwasi wowote unao na msimamizi wa jikoni wa shule yako.

Je, DPS humruhusu mtoto wako kukosa shule kwa sababu ya sikukuu za Kiislamu?

Ndio. Kanuni za Mahudhurio za DPS JHB-R hujumuisha maadhimisho ya kidini kuwa sababu halali ya kukosa shule. Wasiliana mapema na shule yako ili wajue sikukuu inakaribia na mtoto wako hatahudhuria shule.

Je, mtoto wangu anaruhusiwa kuomba shuleni?

Ndio. DPS haibagui dhidi ya wanafunzi kwa misingi ya imani ya kidini, na wanafunzi wanaruhusiwa kuomba na kuendelea na imani yao shuleni ili mradi shughuli hizo haziingilii mazingira ya shule. Tunahimiza familia kuzungumza na viongozi wa shule ili kuhakikisha mahitaji yako ya kidini yanashughulikiwa kwa njia ambayo haitatizi chochote.

Ninaweza kufanya nini wakati mtoto wangu ananyanyaswa kwa kuwa Muisilamu?

Mwanafunzi au mlezi wake anahimizwa kuripoti tukio hilo mara moja kwa kiongozi, mshauri, mwalimu wa shule, au Afisa wa Maafikiano ya Wanafunzi wa wilaya (Ofisi ya Nafasi Sawa kwa Wanafunzi) kwa kuongea au kuandika kwa kutumia fomu ya AC-E2: “Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi/Unyanyasaji. Fahamisha uongozi wa shule ukihisi kuwa tukio hilo linasababisha mazingira yasio salama kwa mtoto wako. Ongea na mtoto wako kuhusu hisia zake, na umsaidie mtoto wako kukumbana na hisia zozote za uwoga au hofu. Wanafunzi wanaweza pia kupiga ripoti kupitia Safe2Tell, nambari ya simu **1-877-542-7233 (Safe2Tell.org)** au kupiga Simu kwa Laini ya usaidizi wa Familia na Jamii, nambari ya simu **720-423-3054**.

Je, wanafunzi wa DPS hupokea mafunzo nyeti ya kitamaduni?

Ndio. Walimu wote wapya wa DPS wanastahili kuchukua saa 1.5 wakipata mafunzo ya uhamasisho kuhusu upendeleo na saa 1.5 ya mafunzo ya kuelewa utamaduni. Wilaya hutoa mipango kadhaa ya hiari, ikiwa ni pamoja na maendeleo ya kibinafsi katika elimu ya kuelewa utamaduni, ambayo ina saa 12 za mafunzo ya msingi na ya juu, mafunzo ya siku mbili yaitwayo DPS ASpire kwa viongozi na wasimamizi wa walimu; na mafunzo ya ya msingi na ya juu ya uhamasisho kuhusu upendeleo kwa wahudumu wote.

Je, DPS hutoa Kiarabu kama chaguo la lugha?

Kwa sasa, Shule ya South High inatoa masomo ya Kiarabu kwa wanafunzi ambao wangependa kujifunza Kiarabu, na hata pia Urithi wa Kiarabu kwa wanafunzi walio na usuli wa lugha ya Kiarabu.

Kuna usaidizi mwingine upi ambao DPS hutoa kwa wanafunzi ambao lugha yao asili ni Kiarabu?

Shule hupewa mwalimu mmoja mtaalamu wa lugha asili kwa kila wanenaji 15 wa lugha asili ili kuunga mkono wanafunzi katika masomo yao ya ELA. Kwa sasa, shule ambazo zina walimu asili wanaoongea lugha ya Kiarabu ni: Denver Green School, Ellis, Hamilton, Holm, McMeen, Merrill, Montclair, Place Bridge, Samuels, South, Joe Shoemaker, Southmoor na University Park.

Je, DPS hutoa huduma za utafsiri na ukalimani kwa wazazi?

Ndiyo, huduma hizi zinatolewa bila malipo kwa wazazi. Ikiwa unahitaji huduma ya utafsiri au ukalimani, tafadhali muulize msimamizi wa shule yako kuwasilisha ombi kwa wakati unaofaa (ikiwezekana siku saba hivi) kwa ofisi ya Huduma za Tamaduni Mbalimbali ya DPS. Kwa mahitaji ya haraka au yasiyotarajiwa, kila shule ina laini ya simu ya ukalimani wa lugha.